## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI MEI, 2023 NA MWELEKEO KWA MWEZI JUNI, 2023.

### Dondoo za tathmini ya Mei, 2023 na mwelekeo wa Juni, 2023:

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Mei, 2023 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa hususan hali ya joto kwa mwezi Juni, 2023 nchini.

i. Katika kipindi cha mwezi Mei, 2023 baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka yalipata vipindi vya mvua sambamba na vipindi vifupi vya mvua kubwa vilivyojitokeza katika maeneo machache.

ii. Mwezi Juni 2023, hali ya joto la chini inatarajiwa kupungua katika maeneo mengi ya nchi ikiashiria kuanza kwa msimu wa Kipupwe (Juni-Agosti), 2023. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya mwambao wa pwani pamoja na maeneo machache ya ukanda wa Ziwa Victoria.

### 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MEI, 2023.

Katika kipindi cha mwezi Mei, 2023 baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka yalipata vipindi vya mvua. Aidha, vipindi vifupi vya mvua kubwa viliripotiwa katika maeneo machache ya ukanda wa Ziwa Victoria, nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa pwani. Mnamo tarehe 28 Mei, 2023 kituo cha Mlingano kilichopo mkoa wa Tanga kiliripoti milimita 89.8 za mvua, ikiwa ni kiwango cha juu zaidi katika mwezi Mei, ikifuatiwa na kituo cha Tanga kilichopima milimita 71.9 mnamo tarehe 28 Mei, 2023 pamoja na kituo cha Matangatuani (Pemba) kilichopima milimita 69.2 za mvua mnamo tarehe 8 Mei, 2023. Vituo vingine vilivyopima mvua zaidi ya milimita 50 ni pamoja na Pemba (67.8 mm) mnamo tarehe 28 Mei, Lyamungu, Kilimanjaro (52.5 mm) mnamo tarehe 2 Mei na Kituo cha Ukiriguru, Mwanza (50.4 mm) tarehe 1 Mei, 2023.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI JUNI, 2023

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto la bahari katika eneo la kati la kitropiki ya bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuwa la juu kidogo ya wastani katika kipindi cha mwezi Juni, 2023. Aidha, eneo la magharibi mwa bahari Hindi linatarajiwa kuwa na joto la bahari la juu ya wastani na eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi, joto la bahari linatarajiwa kuwa la wastani hadi chini ya wastani. Hali hii inatarajiwa kusababisha uwepo wa upepo wenye unyevu unaovuma kuelekea maeneo ya pwani. Kwa upande mwingine, hali ya joto la bahari la juu kidogo ya wastani inatarajiwa katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii inatarajiwa kupunguza uwepo wa upepo wenye unyevu kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Hata hivyo, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kuimarika, hivyo kusababisha Ukandamvua kuendelea kusogea kuelekea kaskazini na kusababisha hewa ya ubaridi kiasi kutoka maeneo hayo ya kusini.

### 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JUNI, 2023

Kipindi cha mwezi Juni 2023, maeneo mengi ya nchi yanatarajiwa kuwa na hali ya joto kiasi hadi baridi ya wastani. Hata hivyo, hali ya baridi ya wastani hadi joto kiasi hususan nyakati za usiku na asubuhi inatarajiwa kujitokeza katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na nyanda za juu Kusini magharibi. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani pamoja na maeneo machache ya ukanda wa Ziwa Victoria. Kwa upande mwingine, vipindi vichache vya upepo mkali vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani.  Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz
**(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)**

727B _01/2022

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 18 °C hadi 26 °C katika maeneo ya mwambao wa pwani na visiwani na kati ya nyuzi joto 14 °C na 22 °C katika maeneo ya nchi kavu. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani hususan katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Juni.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na viwango vya chini ya nyuzi joto 12 °C. Kwa ujumla hali ya ukavu pamoja na vipindi vichache vya mvua inatarajiwa hususan katika maeneo ya miinuko.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 15 °C hadi 20 °C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 15 °C. Kwa upande mwingine, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 °C hadi 20 °C katika maeneo mengi. Kwa upande mwingine, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 11 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz
**(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)**

*727B _01/2022*

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 7 °C hadi 16 °C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko (ikijumuisha mkoa wa Njombe) yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 7 °C. Aidha, hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16 °C hadi 24 °C katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache ya mwambao wa pwani hususan wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 hadi 18 katika maeneo mengi. Maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango chini ya nyuzi joto 12 katika kipindi cha mwezi Juni, 2023. Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi.

## 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI JULAI, 2023

Katika kipindi cha mwezi Julai, 2023 hali ya ukavu na baridi ya wastani inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vifupi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza.

## 2.4 USHAURI

Tahadhari za kiafya zichukuliwe ili kulinda jamii dhidi ya magonjwa yanayoweza kusababishwa na baridi, vumbi na matumizi ya maji yasiyo safi na salama. Kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi katika kipindi hiki, maji na malisho yanapaswa kutumika kwa uangalifu ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Juni, 2023 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz